# K.P.S.E.A
# TATHMINI YA SHULE YA MSINGI
# TATHMINI YA AGOSTI KISWAHILI LUGHA
## Muda: Saa 1 Dakika 40

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

Jina: ______________________________ Shule: ____________________

Nambari ya Tathmini: ______________________________ Tarehe: ______________________________

Nambari ya Shule: ______________________________ Sahihi: ______________________________

**MAELEKEZO KWA WANAFUNZI**

1. Andika jina lako, jina la shule yako na nambari yako ya mthani katika nafasi ulizoachiwa.
2. Andika tarehe,nambari ya shule yako kisa weka sahihi yako.
3. Soma kila swali kwa makini
4. Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote kwenye kijitabu hiki zimepigwa chapa.
5. Jibu maswali yote katika kijitabu hiki.

## JEDWALI LA ALAMA

| SEHEMU | INSHA | LUGHA | KUSI/KUZU | ASILIMIA (%) | KUZ 1 | KUZ 2 | KUF 1 | KUF 2 | KUK 1 | KUK 2 | CHI 1 | CHI12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KIWANGO CHA ALAMA | ALAMA 20 | ALAMA 30 | ALAMA 30 | | 90-100 | 75-89 | 58-74 | 41-57 | 31-40 | 21-30 | 11-20 | 1-10 |
| POINTI | | | | | 8 POINTI | 7 POINTI | 6 POINTI | 5 POINTI | 4 POINTI | 3 POINTI | 2 POINTI | 1 POINTI |
| JUMLA YA ALAMA ZA MWANAFUNZI | | | | | | | | | | | | |

***Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.***

### 1. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Swali la 1 hadi la 5. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

*(Kanini akutana na rafiki yake nyumbani kwao. Ni asubuhi.)*

**Kanini:** He! naona umeamka salama salimini rafiki yangu.
**Mona:** (Kwa mshangao) Umebadilika sana. Mbona huna hata salamu?
**Kanini:** Samahani mwenzangu. Nilivutiwa sana na namna unavyosafisha mazingira. Unafyeka nyasi na naona unazibua mtaro hongera Mona!
**Mona:** (Kwa furaha) Ni jukumu langu kuwasaidia wazazi wangu kuepuka mbu na baadhi ya magonjwa yanayosababishwa na maji taka.
**Kanini:** Yaonekana uliamka mapema sana. Maji yaliyotuama ni makazi ya mbu kuzaana. Mbu husababisha malaria.
**Mona:** Kweli kabisa sasa ndio wakati naenda kula kiamsha kinywa bado sijachelewa. Nataka kuchimba mtaro kuondoa maji yaliyotuama.
**Kanini:** (Akijikuna kichwa) Hayo majani na taka nyingine utazifanya aje?
**Mona:** Nikichoma taka hizo, moshi itachafua mazingira kwa hivyo nitatumia majani na nyasi hizi kutengeneza mbolea.
**Kanini:** Alaa! Taka za plastiki na mikebe utazifanyaje?
**Mona:** Nitazikusanya na kuzirudisha viwandani zitumiwe tena kutengeneza bidhaa. Nashukuru sana kwa kunitembelea. Ushirikiano wetu kutunza mazingira ni kwa manufaa yetu.

1. Kanini angemsalimu Mona namna gani?

A. Shikamoo? B. Habari za jioni?
C. Habari za asubuhi? D. Umeshindaje?

2. Ni jambo gani linaloonyesha kuwa Mona ni mtoto anayewajibika?

A. Anashangazwa na rafiki yake kutomsalimia
B. Anaishi na wazazi wake
C. Anaamka mapema
D. Anawasaidia wazazi wake

3. Kwa nini maji yaliyotuama ni hatari kulingana na mazungumzo?

A. Ni makazi ya mbu kuzaana
B. Watoto wanaweza kuanguka ndani
C. Husababisha baridi katika makazi
D. Ni makazi ya wanyama

4. Ni madhara gani yanayosababishwa na uchomaji wa plastiki?

A. Moshi
B. Uchafuzi wa mazingira
C. Mchanga kukosa rutuba
D. Kuongezeka kwa mbu

5. Mazungumzo haya yanahusu nini?

A. Mbu
B. Mitaro
C. Mazingira
D. Makazi

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Tunapaswa kukabiliana na uhalifu wa aina yoyote. Kuna uhalifu unaoweza kutekelezwa kutokana na kutokuwa na ufahamu wa jambo. Kijiji cha Sijali kilibaki nyuma kimaendeleo. Wakazi wake hawakutilia maanani elimu ya mtoto wa kike. Wavulana tu ndio waliopata nafasi ya kuendelea na masomo. Wasichana walipofika gredi ya sita, saba au nane, waliozwa ili kuletea familia zao mali. Jambo la ajabu ni kuwa mahari waliyopatiwa hayakuwafaa kwa lolote. Takriban wote walitumia fedha zilizolipwa kama mahari na kutumia pesa hizo kwa starehe.

Katika kijiji hiki kulikuwa na mzee mmoja aliyeitwa Hekima. Aliwaelimisha watoto wake wote: wa kike na wa kiume bila kubagua. Wazee wenzake walimcheka na kumdharau kwa kusomesha wasichana. Walimwambia kuwa alipoteza pesa. Mzee Hekima hakukubaliana na mawazo yao. Baada ya miaka michache watoto wake walifuzu vyuoni, wakapata kazi kubwa kubwa. Wakawajengea wazazi wao nyumba ya kifahari na kuwanunulia gari.

Wazee wa Sijali wakashangaa. Wakaamua kuwatunza wana wao na kuwasomesha bila kuwabagua. Wakagundua kuwa wote ni sawa.

6. Je, ni uhalifu gani uliotekelezwa katika kifungu hiki?

A. Kutowasomesha watoto wa kike
B. Kuwasomesha watoto wa kiume
C. Kuleta familia zao mali
D. Wazazi kutowajali wana wao

7. Kwa nini wasichana hawakukamilisha elimu yao?

A. Hawakupenda kusoma
B. Waliozwa mapema
C. Hawakujali elimu yao
D. Walifanya kazi za nyumbani

8. Mali ya watoto walioozwa hayakusaidia familia zao kwa kuwa:

A. Yalikuwa kidogo
B. Wavulana walilipiwa karo
C. Yalitumiwa kwa starehe
D. Yalitumiwa na watu wote kijijini

9. Neno *mahari* limetumika katika kifungu hiki. Mahari ni:

A. pesa au mali yanayotumiwa kwa starehe
B. ng’ombe, mbuzi na kondoo
C. sehemu ambapo mtu huweza kukaa
D. mali inayotolewa kwa wazazi wa mwanamke anayeolewa

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Nyani alitunzwa vyema na wazazi wake. Alikuwa mtoto mtiifu. Alisomea shule ya umma ya Tawe. Alifanya vizuri darasani na hata masomoni. Alifanya vizuri hasa katika mchezo wa kuigiza. Walimu wake akina Twiga walimfunza vyema ili kuhakikisha kuwa yeye na wanafunzi wa wanyama wengine walifua dafu masomoni.

Alikuwa na rafiki mmoja wa karibu, aliisaidia kila aliyetaka msaada wake. Alijiunga na chama cha maskauti ili kutoa huduma ya kwanza kwa wenzake wakati wa michezo. Hili lilimfanya awe na ndoto ya kuwa daktari.

Katika shule ya upili, kipawa chake kilitambulika wazi. Nesi alimshirikisha sana katika utoaji wa huduma ya kwanza kwa wanafunzi waliopata majeraha. Juhudi zake zilimfanya apendwe na kila mtu shuleni. Hatimaye, baada ya kujiunga na chuo kikuu alisomea udaktari. Akawa kielelezo kwa wanyama wenzake. Katika maisha yake ya udaktari, Nyani alijishindia tuzo nyingi sana.

10. Wazazi wa Nyani waliamua kumsaidia kwa kufanya nini?

A. Kumtunza vyema mtoto wao
B. Kutambua kipawa cha mtoto wao
C. Kumsomesha mwanao na wa majirani
D. Kushiriki katika mchezo wa kuigiza

11. Maana ya *kufua dafu masomoni* ni:

A. kuendelea na masomo
B. kuacha masomo
C. kupata maarifa
D. kufanya vizuri masomoni

12. Ni ipi si tabia ya Nyani?

A. Kuwa mtiifu
B. Mwenye bidii
C. Asiyewajali wenzake
D. Mchapa kazi

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Kesho ni siku ya Jumatano. Itakuwa ni sikukuu ya wafanyakazi nchini. Siku hii pia huitwa sikukuu ya Leba. Kwa kawaida sherehe huandaliwa kuadhimisha siku hii. Tatu na Pili watakariri mashairi kuhusu wafanyakazi. Tangu jana wamekuwa wakifanya mazoezi ya kujiandaa. Kesho kutwa watarudi shuleni. Watawaeleza wenzao matukio ya siku hiyo.

13. Ni sherehe gani iliyokuwa ikiandaliwa?

A. Siku kuu ya Mashujaa
B. Sikukuu ya Wajiri
C. Sikukuu ya Leba
D. Sikukuu ya Krismasi

14. Tatu na Pili watarudi shuleni kesho kutwa. Kesho kutwa itakuwa siku gani?

A. Alhamisi
B. Ijumaa
C. Jumamosi
D. Jumatano

15. Tatu na Pili watafanya nini siku ya sherehe?

A. Wataandaa vyakula
B. Watakaribisha wageni
C. Watatunga mashairi
D. Watakariri mashairi

**Soma kifungu kifuatacho Kina nafasi 16 hadi 20. Umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Siti anasomea gredi ya nne. Darasa lao ni ***16*** sana. Kwenye sakafu ***17*** darasa ***18*** kulikuwa na vigae maridadi. Madirisha ya darasa lao ni makubwa na ***19***. Kila siku, wanafunzi ***20*** kupiga deki sakafu ya darasa lao.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 16 | nzuri | mzuri | zuri | lizuri |
| 17 | wa | ya | mwa | kwa |
| 18 | lao | yao | mwao | kwao |
| 19 | linapendeza | wanapendeza | kupendeza | yanapendeza |
| 20 | wamefurahia | walifurahia | watafurahia | hufurahia |

**Kutoka swali la 21 hadi 30, chagua jibu sahihi.**

21. Tambua nomino katika sentensi ifuatayo:

*Mjomba wangu ameingia chumbani.*

A. Mjomba B. ameingia
C. chumbani D. wangu

22. Chagua orodha inayoonyesha vitenzi pekee.

A. Bora, chache, polepole
B. Imba, saidia, penda
C. Sahani, kalamu, nyingi
D. Taratibu, kabisa, sana

23. Maneno haya hufuataana vipi katika kamusi?

i) tutuo
ii) tusi
iii) tasi
iv) tutu

A. (i), (ii), (iii), (iv)
B. (iv), (iii), (ii), (i)
C. (iii), (iv), (i), (ii)
D. (iv), (iii), (i), (ii)

24. Chagua jibu ambalo ni wingi wa sentensi:

*Mkeka wa mhunzi una shimo.*

A. Mikeka ya mhunzi una shimo.
B. Mikeka ya wahunzi wana mashimo
C. Mkeka wa mhunzi yana shimo
D. Mikeka ya wahunzi ina mashimo

25. Ni vifaa gani ambavyo hupatikana nyumbani?

A. Kochi, mlingoti, tumbuu
B. Rula, chati, kabati
C. Balbu, tendeguu, neti
D. Rafu, bendera, mvungu

26. Tegua kitendawili:

*Chaudhi, chachekesha, chapendeza*

A. Kioo B. Sauti
C. Mwavuli D. Utoto, ujana na uzee

27. Maana ya nahau katika sentensi ifuatayo ni:

*Mwalimu alinipa kibali cha kuenda nyumbani.*

A. alinipa muda B. alinihimiza
C. alinikataza D. aliniruhusu

28. Ni kundi gani lililo na nomino zinazopatikana katika ngeli tofauti tofauti?

A. Giza, tunda, mkono
B. Sanara, bata, daktari
C. Figa, majembe, shati
D. Kitambaa, vyoo, chuma

29. Chagua sentensi iliyo na kihisishi.

A. Mwanariadha amesimama kando ya gari lao
B. Nyoso alidondoka lakini hakuumia
C. Nyuki ilifagiwa na upepo jioni
D. Maskini! Mtoto huyu ameumia vibaya

30. Ni maneno gani ya heshima na upole yanayoweza kutumiwa kueleza hali ya mwanamke kwenye picha hii?



A. Mwanamke mnene
B. Mwanamke mwenye mimba
C. Mwanamke aliyejifungua
D. Mwanamke mjamzito

# Answers

**Swali Jibu**

| | |
|---|---|
| 1 | C |
| 2 | D |
| 3 | A |
| 4 | B |
| 5 | C |
| 6 | A |
| 7 | B |
| 8 | C |
| 9 | D |
| 10 | A |
| 11 | D |
| 12 | C |
| 13 | C |
| 14 | A |
| 15 | D |
| 16 | C |
| 17 | B |
| 18 | A |
| 19 | D |
| 20 | D |
| 21 | A |
| 22 | B |
| 23 | C |
| 24 | D |
| 25 | C |
| 26 | B |
| 27 | D |
| 28 | A |
| 29 | D |
| 30 | D |